# TAARIFA KWA WANAFUNZI WASIO NA MAKAO KATIKA SHULE ZA KENTUCKY



## Wanafunzi wanaoishi katika mojawapo ya hali ya maisha zifuatazo wanaweza kustahili kupokea haki na ulinzi fulani chini ya Sheria ya shirikisho la McKinney-Vento:

- Kuishi katika makazi ya muda, moteli, gari, bustani, jengo lililotelekezwa au kambini
- Kuishi nyumba moja na wengine kutokana na upotezaji wa makazi au ugumu wa kiuchumi
- Kuishi katika makazi duni
- Kijana bila mzazi au mlezi (asiye chini ya ulinzi wa mzazi au mlezi)

## Wanafunzi wanaostahiki wana haki ya:

- Kujiandikisha shuleni mara moja, hata bila hati zinazohitajika za uandikishaji
- Kujiandikisha shuleni na kushiriki kikamilifu huku wilaya ya shule ikikusanya hati zinazohitajika
- Kujiandikisa katika shule iliyo karibu na unapoishi au uendelee kusoma shule uliyotoka (shule uliosoma ulipoishi kwa mara ya mwisho ulikuwa na mahali salama na dhabiti pa kuishi au shule ambayo uliandikishwa mara ya mwisho)
    - Iwapo wilaya ya shule inaamini kuwa shule iliyochaguliwa haina manufaa kwa mwanafunzi, basi wilaya lazima impe mzazi, mlezi au mwanafunzi huyo maelezo ya maandishi yanayoeleza msimamo wake na kumjulisha mwanafunzi haki yake ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo
- Kupokea usafiri wa kwenda na kutoka kwa shule ya asili kwa ombi lako
- Kupokea chakula cha shule bila malipo
- Kupata huduma zote za elimu, ambazo zinaweza kujumuisha ushauri nasaha, masomo ya ziada, elimu maalum, programu za vipji maalum na shughuli za ziada za shule

## Ikiwa unaamini kuwa unastahiki, wasiliana na shirika la karibu la watu wasio na makazi haraka iwezekanavyo.

**Mwakilishi wa Mitaa:**
**Simu:**
**Barua pepe:**
**Anwani:**

**Mratibu wa Jimbo:** Zach Stumbo, Ph.D.
**Simu:** (502) 564-1473, ext. 4020
**Barua pepe:** Zachary.stumbo@education.ky.gov
**Anwani:** 300 Sower Blvd. - 5th floor, Frankfort, KY 40601



## Ikiwa unahitaji usaidizi zaidi kuhusu mahitaji yako ya kielimu, wasiliana na Kituo cha Kitaifa cha Elimu kwa Wasio na Makazi (National Center for Homeless Education):

(305) 306-8495 | NCHE.helpline@safalpartners.com | http://nche.ed.gov

Kentucky Department of EDUCATION

*OFFICE OF CONTINUOUS IMPROVEMENT AND SUPPORT*